



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



## TAARIFA KWA UMMA KUHUSUS ASASI ZILIZOPEWA VIBALI VYA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA NA KUTAZAMA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020

**Dar es salaam, 29 Juni, 2020**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawafahamisha wananchi wote kuwa imekamilisha zoezi la uchambuzi wa maombi ya asasi zilizoomba kupewa vibali vya kushiriki katika utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura na utazamaji wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina jukumu la kutoa Elimu ya Mpiga kura; kuratibu na kusimamia wadau wanaotaka kutoa Elimu ya Mpiga Kura nchi nzima. Sheria hii pia inairuhusu kukasimu zoezi la utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura kwa Taasisi na Asasi zenye nia ya kutoa Elimu hiyo. Kwa kuzingatia kifungu tajwa hapo juu, Tume huzialika Asasi zinazokusudia kutoa Elimu ya Mpiga Kura kuhusu michakato mbalimbali ya Uchaguzi kuwasilisha maombi ya kupatiwa vibali vya kutoa Elimu hiyo.

Aidha, Sehemu ya V ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na Sehemu IV ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2020, zimeweka misingi na dhana nzima ya watazamaji wa Uchaguzi nchini. Kanuni hizi zinatoa maelezo kuhusu dhana ya utazamaji wa Uchaguzi na namna Tume inavyotakiwa kusimamia na kuliendesha zoezi hilo.

Hivyo, baada ya Tume kuzialika Asasi kuwasilisha maombi ya vibali kwa tangazo lililotolewa mwezi Novemba 2019, ilipokea maombi kutoka kwa Asasi mbalimbali za Kiraia zilizopo Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Katika uchambuzi wa maombi hayo, Tume ilibaini kasoro kadhaa kama vile: (i) asasi kutosajiliwa kwenye masjala

husika (ii) asasi kutokuwa na ofisi (iii) kushindwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo (mfano: kushindwa kuwasilisha ripoti ya mwaka mwa Msajili wa Mashirika yasiyo ya kiserikali au kushindwa kulipa ada ya mwaka) (iv) baadhi ya asasi kuwasilisha maombi ya kutoa elimu ya uraia badala ya elimu ya mpiga kura (v) baadhi ya asasi kuwasilisha maombi bila kueleza maeneo wanayotaka kutoa elimu ya mpiga kura (vi) malengo ya asasi kutoendana na zoezi la utoaji elimu ya mpiga kura (vii) baadhi ya asasi kutowasilisha nyaraka muhimu kama vile katiba, cheti cha usajili na ratiba ya zoezi la utoaji elimu ya mpiga kura (viii) asasi kutowasilisha orodha kamili ya majina ya watendaji wakuu (ix) asasi kutoonyesha njia za mawasiliano hususan namba za simu.


Baada ya uchambuzi wa maombi hayo, Tume imeridhia kutoa vibali kwa Asasi 245 zilizokidhi vigezo vilivyowekwa kwa ajili ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura na Asasi 97 kwa ajili ya kushiriki utazamaji wa Uchaguzi Mkuu.

Tume inazitaka Asasi zote zilizopewa vibali kuzingatia taratibu na kanuni zinazoongoza mazoezi hayo ukiwemo mwongozo wa utoaji Elimu ya Mpiga kura. Kwa muktadha huo, Asasi zote zilizopewa vibali kwa ajili ya kutoa Elimu ya Mpiga Kura zitalazimika kushiriki katika semina maalum ya kuupitia mwongozo huo.

Vilevile, Tume inazitaka Asasi zilizopewa vibali kuwasilisha orodha kamili ya watendaji watakaoshiriki zoezi la utoaji elimu/utazamaji wa Uchaguzi, kuonyesha maeneo halisi watakayotoa elimu ya mpiga kura/kutazama Uchaguzi na kuainisha vyanzo vya fedha.

Orodha kamili ya asasi zilizopewa vibali itatangazwa kupitia vyombo vya habari na itapatikana pia kwenye tovuti ya Tume ([www.nec.go.tz](http://www.nec.go.tz)).

Imetolewa na:

  
Mkurugenzi wa Uchaguzi

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**